# Dk. Mwigulu aonya bidhaa bandia zinavyoharibu maisha

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu Dk. Mwigulu Nchemba amesema Serikali itaendelea kupambana na biashara ya bidhaa bandia kwa kuwa zinakwamisha ukuaji wa viwanda, sekta binafsi pamoja na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Pia, Waziri Mkuu amesema Serikali itachukua hatua kali kwa wawekezaji wanaofanya utapeli na uhujumu uchumi kwa kuanzisha kampuni kwa kutumia majina ya Watanzania huku kampuni hizo zikiwa ni za kwao jambo ambalo halikubaliki.

Ametoa kauli hiyo jana alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye ufunguzi wa Kituo cha Huduma za Magari cha Superdoll na Chuo cha Mafunzo ya Usafiri na Usalama Barabarani kilichopo jijini Dodoma.

Aidha, Dk. Mwigulu amesema bidhaa bandia zinakwamisha jitihada za ujenzi wa viwanda na kukuza sekta binafsi na pia zimekuwa chanzo cha ajali, hasara za kiuchumi na wakati mwingine zinasababisha vifo na ulemavu wa kudumu kwa wananchi, hivyo hakuna nafasi ya kuendelea kuvumilia vitendo hivyo.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amesema Serikali itaendelea kufuatilia na kuwachukulia hatua kali wawekezaji wanaofanya vitendo vya udanganyifu, uvunjifu wa sheria na hujuma dhidi ya uchumi wa Taifa kwa kufungua makampuni kwa kutumia majina ya wazawa.

Waziri Mkuu ameyasema hayo baada ya Serikali kubaini kuwepo kwa baadhi ya wawekezaji wanaotumia majina na taarifa za Watanzania kuanzisha kampuni za kizawa kwa lengo la kupata fursa zinazotengwa kwa wazawa, ilhali umiliki na manufaa yote ya kampuni hizo hubaki mikononi mwao.

Awali, Waziri Mkuu alizitaka taasisi zote za Serikali kuhakikisha zinatumia vipuri halisi ili kupunguza gharama za matengenezo, kuongeza usalama wa vyombo vya moto na kuepuka matumizi ya bidhaa bandia katika shughuli za Serikali.

Akizungumzia ushiriki wa Watanzania katika uchumi wa nchi yao, Waziri Mkuu amesema Tanzania inaendelea kuthamini mchango wa wawekezaji na sekta binafsi, lakini haitakubali vitendo vya ubinafsi vinavyowanyima Watanzania fursa walizostahili kwa mujibu wa sheria.

Pia, Waziri Mkuu ameipongeza kampuni ya Superdoll kwa uwekezaji huo mkubwa akisema ni ushahidi kuwa Watanzania wana uwezo wa kujenga, kuendesha na kukuza kampuni zinazoweza kushindana katika viwango vya kimataifa huku zikichangia ajira, mafunzo ya ujuzi na maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Amesema kituo hicho tayari kimechangia kutoa mafunzo kwa zaidi ya vijana 100 na kutoa ajira kwa mamia ya Watanzania wakati wa utekelezaji wa mradi huo. "Serikali imejivunia kuona kampuni za Kitanzania zilizojengwa na Watanzania, zinaendeshwa na Watanzania na zinaendelea kuwekeza kwa ajili ya Watanzania wote."

Kwa upande wake, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema uwekezaji huo utachangia kuimarisha usalama barabarani, kuongeza ujuzi wa madereva na wataalamu wa usafiri, kuendeleza matumizi ya teknolojia za kisasa na kuandaa rasilimali watu wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira la kikanda na kimataifa.

Profesa Mbarawa pia alieleza umuhimu wa kuendelea kuboresha mazingira ya matumizi ya teknolojia mpya katika sekta ya usafirishaji, ikiwemo matumizi ya matairi ya "super single", ili kuongeza ushindani wa wasafirishaji wa Tanzania katika masoko ya kikanda.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Superdoll, Seif Ali Seif amesema kituo hicho ni sehemu ya utekelezaji wa maono ya Rais Dk. Samia kuendelea kuimarisha uwekezaji, huduma za kisasa, mafunzo na usalama katika sekta ya usafirishaji nchini.

# Serikali yaongeza kasi ya mageuzi ya kidijitali

Na Asha Mwakyonde, *DODOMA*

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Profesa Riziki Shemdoe, amezindua mifumo ya kidijitali ya Serikali ya Government Service Directory (GSD) na Mfumo wa NGAO, huku akisisitiza kuwa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ni nguzo muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma za umma, kuimarisha uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa taasisi za Serikali.

Profesa Shemdoe aliipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa juhudi zake za kusimamia na kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali serikalini, ambapo alisema mchango wake umewezesha taasisi nyingi za Umma kuunganishwa na kubadilishana taarifa kwa ufanisi. hatua ambayo imekuwa msingi muhimu wa kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi, kuongeza uwazi na kuharakisha utekelezaji wa majukumu katika taasisi za serikali.

Profesa Shemdoe alizindua mifumo hiyo wakati wa kufunga Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026 yaliyofanyika juzi katika viwanja vya Chinangali jijini hapa ambapo alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuwekeza katika mifumo ya kidijitali ili kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani.

Alisema mfumo wa Government Service Directory (GSD), utarahisisha wananchi kupata taarifa za huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali kupitia dirisha moja, ikiwemo mahitaji ya kupata huduma, muda wa huduma kutolewa, gharama husika pamoja na maeneo yanayotoa huduma hizo.

"Mfumo huu ni hatua muhimu katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa urahisi, uwazi na kwa wakati, huku ukichochea uwajibikaji kwa taasisi za umma," alisema Prof. Shemdoe.

Aidha, alizitaka taasisi zote za umma kuhakikisha mifumo wanayoibuni au kuitumia ina uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya Serikali kupitia miundombinu ya Serikali mtandao ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma.

Katika hatua nyingine, Prof. Shemdoe alieleza kuwa Mfumo wa NGAO umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa mifumo ya kidijitali ya Serikali kwa kutumia teknolojia ya uthibitishaji wa nywila ya muda mmoja (One Time Password - OTP), hatua itakayosaidia kulinda taarifa muhimu dhidi ya vitisho vya usalama wa mtandao.



*Waziri Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia) alipomwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye ufunguzi wa Kituo cha Huduma za Magari cha Superdoll na Chuo cha Mafunzo ya Usafiri na Usalama Barabarani kilichopo jijini Dodoma, jana.*

# TAKUKURU yamkamata aliyekimbia kifungo cha miaka 20

Na Mwandishi Wetu

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha imethibitisha kumkamata na kumrejesha mkoani hapa mshtakiwa Amani Elifatio Mlay, aliyekuwa Mratibu wa TASAF wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, baada ya kutoroka mahakamani siku ya kutolewa hukumu dhidi yake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa leo na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Arusha, Zawadi Ngailo, mtuhumiwa huyo alikamatwa Jumapili, Juni 21, 2026 katika eneo la Mangaka wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara, kufuatia msako uliofanywa baada ya kutoweka akiwa nje kwa dhamana katika shauri la jinai lililokuwa likisikilizwa Mahakama ya Wilaya ya Arusha.

TAKUKURU ilieleza kuwa Amani alikuwa akikabiliwa na makosa sita, yakiwemo manne ya kutumia nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri wake, kinyume na sheria za kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na sheria za uhujumu uchumi.

Makosa hayo yanadaiwa kufanyika wakati akiwa Mratibu wa TASAF, ambapo alitengeneza nyaraka zenye taarifa za uongo zikionesha kuwa mzabuni alikuwa amewasilisha vifaa vya ujenzi kwa ajili ya mradi wa uzio wa Shule ya Msingi Shangarao katika Jiji la Arusha.

Kwa mujibu wa ushahidi uliowasilishwa mahakamani, nyaraka hizo zilihusisha vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh milioni 64.2.

Mahakama ilimtia hatiani Januari 16, 2026 katika makosa manne na kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 20 jela.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alitoroka siku ya kutolewa hukumu, hali iliyosababisha mahakama kutoa hati ya kukamatwa kwake ili akamatwe na kupelekwa kutumikia adhabu hiyo.

Ngailo amesema baada ya kukamatwa, taratibu za kumfikisha mahakamani zinaendelea ili asomewe hukumu hiyo na kuanza rasmi kutumikia kifungo alichopewa.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na TAKUKURU kwa kutoa taarifa za wahalifu wa vitendo vya rushwa na ubadhirifu, akisisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kuwafuatilia watuhumiwa popote walipo hadi wakamatwe na kufikishwa mbele ya sheria.